**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA DAWATI LA SEKTA BINAFSI

**(*PRIVATE SECTOR DESK*)**

**KUANZIA OKTOBA 2018 HADI JANUARI 2020**




**Januari, 2020**

**YALIYOMO**

YALIYOMO ........................................................................................................2
1.0 CHIMBUKO NA VIPAUMBELE VYA UTEKELEZAJI ..................................................3
1.1 UTEKELEZAJI WA KAZI ZA DAWATI ..............................................................4
1.2 TAFITI ...........................................................................................................4
1.3 MATOKEO YA TAFITI SEKTA YA MIFUGO ............................................................5
1.3.1 Matokeo ya Tafiti ya mnyororo wa thamani wa maziwa .....................................6
1.3.2 Matokeo ya tafiti mnyororo wa thamani wa nyama ............................................8
1.3.3 Matokeo ya tafiti mnyororo wa thamani wa ngozi (2018/19) ..............................8
1.3.4 Matokeo ya tafiti mnyororo wa thamani wa kuku ..............................................9
1.3.5 Matokeo ya tafiti mnyororo wa thamani wa vyakula vya mifugo ........................10
1.4 MATOKEO YA TAFITI SEKTA YA UVUVI ............................................................11
1.4.1 Matokeo ya Tafiti ya mnyororo wa thamani uvuvi wa Bahari Kuu.......................12
1.4.2 Matokeo ya utafiti wa Ukuzaji wa Viumbe Maji ...............................................12
2.0 UPATIKANAJI WA MIKOPO KWA WAFUGAJI NA WAVUVI ....................................13
2.2 Vyama vya Ushirika vya Wavuvi ....................................................................15
2.3 Vyama vya Ushirika vya Mifugo .....................................................................17
3.0 KUTANGAZA FURSA NA KUTATUA CHANGAMOTO ZA UWEKEZAJI NA BIASHARA ..........20
3.1 Wadau Waliohudumiwa na Dawati ..................................................................20
3.2 Mashirikiano katika Utendaji...........................................................................20
3.3 Makubaliano ya Viwanda vya Kimkakati vya Maziwa ...........................................20
3.4 Kiwanda cha AZAM .............................................**Error! Bookmark not defined.**
3.5 Aquasol Limited..................................................**Error! Bookmark not defined.**
3.6 Viwanda vya Samaki vya Kanda ya Ziwa ..........................................................21
3.7 Chakula cha Mifugo .............................................**Error! Bookmark not defined.**
3.8 Uvuvi katika EEZ ..........................................................................................21
3.9 Tathmini ya Zao la Ngozi .....................................**Error! Bookmark not defined.**
3.10 Kiwanda cha nyama cha TANCHOICE ............................................................22
4.0 KUITANGAZA SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI .....................................................25
4.1 Ushiriki katika maonesho ...............................................................................25

## 1.0 CHIMBUKO NA VIPAUMBELE VYA UTEKELEZAJI

Utekelezaji wa kazi za Dawati la Sekta Binafsi kwa Mwaka 2019/20 linatokana na: -

Kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa **John Pombe Joseph Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa kampeni za uchaguzi za mwaka 2015 na hata baada ya kuchaguliwa ameahidi kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Kutekeleza IIlani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015-2020, Ibara ya **25** (***a – q***) kwa upande wa Mifugo na Ibara ya **27** (***a-p***) kwa upande wa uvuvi.

Kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili (Five Year Development Plan II - FYDP II), 2016-2021; na

Kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (Agriculture Sector Development Programme – ASDP II), Sera ya Mifugo (2006) na Sera ya Uvuvi (2015).

## 1.1 UTEKELEZAJI WA KAZI ZA DAWATI

| NO | MALENGO | Kazi Mahsusi za Utekelezaji | Viashiria |
|---|---|---|---|
| 1 | Kufanya tafiti | Kushirikiana na sekta binafsi kufanya tafiti za minyororo ya thamani ili kubaini fursa na maeneo ya uwekezaji | Idadi ya tafiti za minyoro ya mazao ya kisekta zilizofanyika |
| 2 | Upatikanaji wa mikopo kwa wafugaji na wavuvi | Kuhamasisha vyama vya ushirika na kuviunganisha na taasisi za fedha kwa ajili ya mikopo | Idadi ya vyama vya ushirika vitakavyopata mikopo |
| | | Kuhamasisha taasisi za wizara, wafugaji na wavuvi kwa ajili ya kufanya shughuli zao kibiashara ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha na taasisi za kifedha | Taasisi za mifugo na uvuvi kuanza kujiendesha kibiashara na kupata mikopo |
| | | Kutoa ushauri wa kitaalamu wa upatikanaji wa mikopo/lease financing, maandiko ya biashara, taasisi za dhamana kama PASS na Bima | Idadi ya maandiko ya uvuvi na zana za uzalishaji na dhamana za ukopaji |
| 3 | Kuitangaza sekta ya mifugo na uvuvi | Kushiriki warsha, makongamano, maonesho, mikutano, vipeperushi, mabango, na kutangaza fursa kupitia vyombo vya habari kama magazeti, TV, radio na mitandao ya kijamii | Idadi ya matangazo, vipeperushi na mikutano ya kutangaza fursa |
| 4 | Kufanya tathmini na ufuatiliaji (Monitoring and Evaluation) | Kuandaa viashiria vya tathmini na ufuatiliaji | Aina ya viashiria vya tathmini na ufuatiliaji |
| | | Kufanya tathmini na ufuatiliaji kuendana na *logical frame work* | *Logical frame work* kutumika katika kufanya tahmini na ufuatiliaji |
| | | Kuandaa mikutano ya wadau katika Dawati ili kutathmini utekelezaji wa utekelezaji | Idadi ya mikutano ya wadau |

## 1.2 TAFITI

Katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Dawati la Sekta Binafsi kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi, Taasisi za Serikali tulifanya tafiti nane (8) ambazo ni:-

I. Tathmini ya gharama na faida katika mnyororo wa thamani wa maziwa

II. Mnyororo wa thamani wa zao la maziwa

III. Mnyororo wa thamani wa zao la nyama

IV. Mnyororo wa thamani wa zao la Ngozi

V. Mnyororo wa thamani wa kuku

VI. Mnyororo wa thamani wa vyakula vya viwandani vya mifugo (compound feeds)

VII. Mnyororo wa thamani wa ukuzaji viumbe maji

VIII. Mnyororo wa thamani wa samaki

Kielelezo Na 1 Mazao yaliyofanyiwa utafiti


1. Maziwa


2. Nyama


3. Kuku


4. Ngozi


5. Chakula cha Mifugo


6. Uvuvi


7. Ukuzaji Viumbe Maji


## 1.3 MATOKEO YA TAFITI SEKTA YA MIFUGO


Idadi ya mifugo Tanzania

| | | | |
|---|---|---|---|
|  | Idadi ya ng'ombe: milioni 32.5 |  | Idadi ya kondoo: milioni 5.5 |

| | | | |
|---|---|---|---|
|  | Idadi ya Mbuzi: milioni 20 |  | Idadi ya kuku wa kisasa**:** milioni **40.6** |
|  | Idadi ya kuku wa kienyeji**:** milioni **38.5** |  | Idadi ya punda: 636,997 |

### 1.3.1 Matokeo ya Tafiti ya mnyororo wa thamani wa maziwa

| | | |
|---|---|---|
|  | • Idadi ya ng'ombe wa maziwa mil 6.95 kati ya hawa wa kisasa ni **1,294,882**<br>• Uzalishaji wa maziwa kwa mwaka: bilioni lita **2.7** ambapo:<br>✓ Lita milioni **900** toka kwa ng'ombe wa kisasa **(1/3)**<br>✓ Lita bilioni **1.8** kutoka ng'ombe wa asili (2/3) | • Kuzalisha kwa tija (Malisho bora, afya ya mnyama na kuboresha mbaari- *improved breed*)<br>• Kupunguza gharama za uzalishaji haswa chakula zinazochangia 25% ili kupata faida. |

| | | |
|---|---|---|
|  | • **Usindikaji**:<br>• Viwanda**: 99** (Viwanda vikubwa 5)<br>• Uwezo: lita milioni **276.5** kwa mwaka<br>• Usindikaji kwa sasa: lita milioni **70** kwa mwaka | •Kuongeza usindikaji zaidi ya asilimia 50 ya uwezo wa viwanda, kupunguza ushindani wa maziwa yasiyo rasmi (97%) ili kuongeza soko na uingizaji wa maziwa ya unga |
|   | •Unywaji maziwa: lita **47** kwa mtu kwa mwaka<br>•Mapendekezo ya FAO: lita **200** kwa mtu kwa mwaka | •Mpango wa unywaji maziwa mashuleni na mikakati ya masoko |
|   | •Mstari wa juu unaonyesha ongezeko la maziwa yanayoingizwa, UHT imepungua (msatari wa chini) na maziwa ya unga yanaendelea kupanda. (Msatari wa kati) | •Kuangalia sera ya uingizwaji wa maziwa ya unga bila kuathiri malighafi hiyo (Kujua kiasi cha maziwa yanayoitajiwa na viwanda na kuagiza kwa pamoja) |

### 1.3.2 Matokeo ya tafiti mnyororo wa thamani wa nyama

| | | |
|---|---|---|
|  | •Idadi ya wafugaji: kaya milioni **4.6**<br>•Wanyama hai wanaouzwa kwa mwaka; ng'ombe milioni **2.3, mbuzi milioni 2**; kondoo milioni **0.4** | •Uboreshaji wa kosaafu za mifugo ya asili ili kuongeza tija |
|  | •Ulaji wa nyama kwa mwaka: kilo **15**<br>•Ulaji wa nyama unaopendekezwa na FAO: kilo **50** | •kuhamasisha ufugaji bora wa kibiashara katika mfumo wa ranchi na kuboresha malisho |
|  | ▪ Viwanda : **32**<br>• Uwezo kwa mwaka: tani **626,992**<br>•Uzalishaji/mwaka: **tani 81,220** | •Kuendeleza utambuzi na usajili wa mifugo na kuweka mfumo wa ufuatiliaji |
|  | •Uzalishaji wa nyama kwa mwaka: tani **690,629**<br>•Mahitaji: tani milioni **1.62**<br>•Uchinjaji (*offtake*): asilimia **8-10 kwa mwaka**<br>•Uzito (Carcas weight): kilo **100-175** kwa ng'ombe | |


### 1.3.3 Matokeo ya tafiti mnyororo wa thamani wa ngozi (2018/19)

| | | |
|---|---|---|
|  | **Uzalishaji**<br>•Tani 16,012 kwa mwaka<br>•Viatu jozi milioni 1.2 | |

| | | |
|---|---|---|
|  | • Mahitaji : jozi milioni 54 kwa mwaka | |
|  | **Viwanda**<br>•Idadi 9<br>•Uwezo: Ngozi milioni 17.6 kwa mwaka<br>•Uzalishaji : Ngozi milioni 2.8 kwa mwaka | •Serikali isimamie upigaji chapa sahihi, uchinjaji, uchunaji, uhifadhi, madaraja na utunzaji wa ngozi;<br>•Serikali itoe motisha kwa uwekezaji (Mazingira ya biashara) |
|  | Usafirishaji nje kwa mwaka<br>•Ngozi ya *Wet blue* : tani 5.4, Mapato: US$ milioni 3.6<br>•Ngozi ghafi: tani 3.6, Mapato: US$ 2 mil<br>•Nchi/Masoko: China, Kenya, Ethiopia, Pakistan, Nigeria | •Kubaki na tozo ya 10% (wet blue) kama ilivyoainishwa kwenye nchi za EAC<br>•Pia kubaki na asilimia 80 au ongezeko ili kulinda viwanda vya ndani. |
|  | **Uagizwaji wa viatu**<br>•Jozi milioni 50 kwa mwaka<br>•Mrahaba: US$ milioni 39.13<br>•Kutoka: China, Italy, Kenya | •Kuongeza tozo za bidhaa za ngozi zinazoingizwa na kuboresha utaalam wa ndani wa uzalishaji. |

**1.3.4 Matokeo ya tafiti mnyororo wa thamani wa kuku**

| | | |
|---|---|---|
|  | •Wafugaji: milioni **3.7**<br>•Idadi ya kuku: milioni **79.1**<br>• Kuku wa asili: milioni **38.5** | •Kuongeza uzalishaji wa kuku wazazi.<br>•Kuzalisha virutubisho vya kutengenezea vyakula |

| | | |
|---|---|---|
| | • Kuku wa kisasa: milioni **40.6** | vya kuku ndani ya nchi ili kupunguza gharama za vyakula |
|  | •Ulaji wa nyama ya kuku: kilo **2.07** kwa mtu/mwaka<br>•Ulaji wa mayai: 1**06** kwa mtu/mwaka | |
|  | •Uzalishaji wa mayai: bilioni **3.6** kwa mwaka<br>•Uzalishaji wa vifaranga | |
|  | •Viwanda: **10**<br>•Uwezo: kuku **39,800** kwa siku | |

## 1.3.5 Matokeo ya tafiti mnyororo wa thamani wa vyakula vya mifugo

| | | |
|---|---|---|
|   | •Mahitaji : tani milioni **2** kwa mwaka<br>•Uzalishaji: tani **520,000 (26%)**<br>•Viwanda: **94**<br>•Vikubwa: **50**<br>•Vya kati: **44** | •Kutoa motisha kwa wawekezaji kwenye vyakula vya mifugo<br>•Kusimamia ubora wa vyakula |


| | | |
|---|---|---|
|  | •Uagizaji wa vyakula, malighafi na vichechemuzi Kutoka nchi za Uholanzi, Ubelgiji na Malawi | |

## 1.4 MATOKEO YA TAFITI SEKTA YA UVUVI


| | | | |
|---|---|---|---|
|  | •Idadi ya Wavuvi : **202,053** |  | •Uzalishaji tani **389,459.4**<br>•Maji baridi tani **85.7**%<br>•Maji chumvi **14.3**% |
|  | •Usafirishaji nje: tani **38,114**<br>•Mapato: US$**15.6 M**<br>•Kwenda: Uarabuni, Japan Rwanda, Malawi, Congo, Nchi za Ulaya, Israeli |  | •Ulaji wa samaki kwa mwaka: **8.2 kg**<br>•Mapendekezo ya FAO: kilo 20.3 kwa mtu/mwaka |
|  | •Uingizwaji: tani **22,752**<br>•Mrabaha: US$ **12.9** M<br>•Kutoka: China, | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Japan | | |

### 1.4.1 Matokeo ya Tafiti ya mnyororo wa thamani uvuvi wa Bahari Kuu

| | | |
|---|---|---|
| •  | | |
|   | •Uvuvi wa Bahari Kuu unafanywa sana na meli za kigeni. Uvuvi wake hasa ni wa samaki aina ya jodari na aina zake kama inavyoonyesha katika chati katika kipindi cha mwaka 2001-2014. | •Taifa liwe na meli za uvui wa bahari kuu,<br>Ujenzi wa bandari |


### 1.4.2 Matokeo ya utafiti wa Ukuzaji wa Viumbe Maji


| | | |
|---|---|---|
|   | •Idadi ya wafuga samaki: **27,742**<br>•Idadi ya mabwawa: **26,445**<br>•Idadi ya vizimba: **408**<br>•Uzalishaji: tani**18,081.6**<br>•Vifaranga: **17,422,776**<br>•Mashamba: Binafsi **17** vifaranga 16,822,776<br>•Serikali **3** vifaranga 600,000<br>•Lengo: uzalishaji vifaranga | •Kutoa kodi ya zana za uzalishaji katika ufugaji wa samaki<br>•Kuwekeza katika uzalishaji wa vyakula na vifaranga bora vya samaki<br>•Kupanga maeneo ya ufugaji smaki katika vizimba na kufanya tathmini ya athari ya kimazingira |


| | | |
|---|---|---|
| | ifikapo mwaka 2025<br>• Mashamba: Binafsi vifaranga milioni 45<br>• Serikali vifaranga milioni 15 | |

## 2.0 UPATIKANAJI WA MIKOPO KWA WAFUGAJI NA WAVUVI

Kwa muda mrefu sekta ya mifugo na uvuvi imekuwa ikipata asilimia chini ya mbili ya mikopo ya sekta ya Kilimo (TADB, 2018). Hivyo, tumeunganisha wadau na Taasisi za kifedha ikiwa na kutangaza fursa zilizopo katika mabenki. Dawati limefanya vikao na Benki za TADB, CRDB, NMB, NBC, TPB, na Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF). Katika vikao hivi baadhi ya mabenki yalionyesha changamoto kwa kukosekana kwa mikopo kwa wafugaji wadogo wadogo, wavuvi na vyama vya ushirika ni kutokana na kutokuwa na muundo wa kuwatambua kutokana na shughuli zao kuwa za kuhama hama. Kwa sasa tunafanya majaribio ya mfumo unaoitwa 'UVUVI DATA BASE' ambao umeshasajili wavuvi Zaidi ya 557 wa Mwanza, Geita na Kigoma.





Picha za Uvuvi Data Hub (Majaribio)

Pia ufuatiliaji wa huduma za dhamana zinazotolewa na PASS, African Guarantee Fund (TADB), EFTA (Lease financing) na Shirika la Bima la Taifa umefanyika.

Katika kipindi cha Oktoba 2018 hadi Jan. 2020 kiasi cha maombi ya mikopo na mifugo ni bilioni 104.5. Kiasi kilichotolewa hadi sasa ni bilioni 12. Zaidi ya asilimia 99.9 imetolewa kwa makampuni na watu binafsi na asilimia ilobakia 0.1 imetolewa kwa vyama vya ushirika vya mifugo na uvuvi asilimia sifuri.

Hivyo vyama vya ushirika kuonekana kotokuwa na nafasi kubwa kwenye uwekezaji kuelekea uchumi wa viwanda na kuondoa umasikini.

Jumla ya Mikopo iliyotolewa




2.1 Kuhamasisha vyama vya ushirika na kuviunganisha na taasisi za fedha kwa ajili ya mikopo

## 2.2 Vyama vya Ushirika vya Wavuvi

Kuna Vyama vya Ushirika vya Wavuvi 116, kati ya hivyo, vilivyohai ni vyama 89 sawa na asilimia **76**.

## UPATIKANAJI WA MIKOPO

Uratibu wa ufunguzi wa “Mvuvi Account” katika Benki ya TpB kwa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wavuvi Tanzania (CHAKUWATA) ulifanyika ili kusaidia wadau wa uvuvi kuweka akiba na kupata mikopo na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Uhamasishaji unaendelea kwa wavuvi waweze kutumia fursa hii.




*Naibu waziri wa Mifugo na Uvuvi Mh. Abdallah Ulega akionyesha mfano wa kadi ya Mvuvi katika Hafla iliyofanyika katika mwalo wa Igombe tarehe 23/09/2019*

Aidha, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi inaendelea kuunganisha vyama vya Ushirika **39** vya Wavuvi na taasisi za kifedha ili waweze kupata mikopo.



*Waziri wa mifugo na uvuvi Mh. Joelson Mpina akionyesha hati ya usajili wa chama cha ushirika wa Igombe kwenye uzinduzi kanda ya Ziwa. (Oktoba, 2019)*

## 2.3 Vyama vya Ushirika vya Mifugo

Kuna Vyama vya Ushirika vya Mifugo 89, kati ya hivyo, vilivyohai ni vyama 35 sawa na asilimia **35**.

**UPATIKANAJI WA MIKOPO**

TADB imeidhinisha mkopo kwa TDCU jumla ya Tshs. **237,970,000**/= kwa vyama vya CHAWAMU na UWAMWA kwa ajili ya ng'ombe bora **76** na ujenzi wa mabanda bora **25** ambao umekuwa ukitolewa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa ng'ombe.

Dawati limewatembelea UWAMWA baada ya kupokea ng'ombe hao **25**, ng'ombe wote wana mimba za miezi mitatu hadi saba na wanatarajia kutoa lita za maziwa kati ya **15** na **20** kwa siku kulingana. Hata hivyo, taarifa za ubora na uzalishaji wa maziwa zitapatikana baada ya ng'ombe hao kuzaa na kuanza kukamuliwa na hii itategemea kwa asilimia kubwa matunzo watakayopatiwa ng'ombe hao ikiwa ni pamoja na malisho na huduma za afya.

Chama cha Wafugaji Muheza (CHAWAMU) wameshapokelewa ng'ombe 25 bado ng'ombe **26**. Ng'ombe wote hawa kwa vyama vyote viwili wamepetikana kutoka kwa wafugaji wa Wilaya ya Rungwe.



*Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega akiwasikiliza kwa makini baadhi ya wanachama wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Ng'ombe wa Maziwa Mkoa wa Tanga (TDCU). Pembeni ya Naibu Waziri ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga Bw. Martine Shigella (21.10.2019)*

**Kuhamasisha taasisi za wizara, wafugaji na wavuvi kwa ajili ya kufanya shughuli zao kibiashara ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha na taasisi za kifedha;**

Dawati limeshiriki katika kuratibu na kupitia Maandiko ya Biashara (Business Plans) ya TVLA, NARCO, TAFICO na TALIRI ili kuweza kuwasilishwa katika Benki za Uwekezaji na Biashara. Maandiko ya Biashara ya NARCO na TALIRI yamewasilishwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB). Aidha, Andiko la TAFICO liko katika hatua za mwisho za ukamilishaji baada ya Mtalaam Mwelekezi kupatiwa vipengele vya masahihisho na Wizara. Aidha tunaendelea kufuatilia mwenendo wa mikopo hiyo kwa kushirikiana na benki ya TADB kanda ya kati (Dodoma)

**Kutoa ushauri wa kitaalamu wa upatikanaji wa mikopo/lease financing, maandiko ya biashara, taasisi za dhamana kama PASS na Bima;**

**Huduma ya bima**

Benki ya Posta Tanzania na Shirika la Bima la Taifa (NIC) wanaendelea na mchakato wa maandaliza ya utoaji wa bima ya mifugo na uvuvi ambayo itakuwa inatumika kama dhamana wakati wa uombaji wa mikopo. Kwa sasa NIC wapo kwenye hatua ya kusaini *treaty (Jan. 2020)* ili kuendelea na taratibu za upatikanaji ya huduma ya bima.

**Dhamana za TADB**

Kwa upande wa dhamana ya TADB kupitia dhamana ya AGF ambayo inadhamini asilimia 50 ya dhamana bado haijaweza kutumiwa na wafugaji na wavuvi hivyo maongezi yanaendelea juu ya kuboresha huduma hii. Kikao cha mwisho kilifanyika tarehe 21/01/2020

**Dhamana za PASS**

Kwa upande wa PASS juhudi tunaendelea kuwaunganisha wadau wenye changamoto ya dhamana ikiwa pamoja na Ushirika wa watengenezaji wa bidhaa za Ngozi (TALEPA) na vyama vya ushirika wa maziwa Tanga (TDCU).

Mfano wa utaratibu wa dhamana ya PASS kwa mkopaji wa million 500 ambao hutoa asilimia 60 ya dhamana ni kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 2 hapa chini

Jedwali Na. 2 Utaratibu wa dhamana ya PASS

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kiasi cha mkopo** | **500,000,000.00** | 0.13 | | |
| **Makato** | | | | |
| Gharama za kuomba (*Application fee*) | 0.625% | 500,000,000 | 3,125,000.00 | |
| Gharama za andiko la biashara | 1.300% | 500,000,000 | 6,500,000.00 | |
| *Gharama ya dhamana (Quarantee fee (after loan approval)* | 1.300% | 500,000,000 | 6,500,000.00 | |
| Riba *(Interest fee (pa reducing))* | 13.000% | 500,000,000 | 65,000,000.00 | |
| Dhamana | 500,000,000.00 | 325,000,000.000 | 325,000,000.00 | Mchango wa mkopaji 65% |
| **Kiasi cha mkopo** | **500,000,000.00** | | | |

### *Lease financing* (EFTA)

Wakopaji wa vifaa/pembejeo vya mifugo na uvuvi wanaweza pata zana kupitia mikopo ya EFTA ambapo hulipa malipo ya awali ya asilimia 20 hadi 30 na kifaa kilichonunuliwa hutumika kama dhamana.

Tunaendelea kuunganisha wadau wenye mahitaji hususani wale wenye changamoto ya dhamana na wanahitaji vifaa.

### Kufuatilia hali ya mikopo ya wafugaji na wavuvi kwenye taasisi za fedha;

Katika kipindi cha Oktoba 2018 hadi Januari 2020 jumla ya mikopo ya mifugo na uvuvi imefikia Tshs. Bil. 104.46 ambayo ipo kwenye hatua tofauti. Mikopo iliyotolewa na kupitishwa (*Approved)* ni Tshs. Bil 26.15 (bilioni 23.5 mifugo na bilioni 2.6 Uvuvi) na mikopo iliotolewa ni Tshs bilioni 12 (bilioni 11.7 Mifugo na milioni 323.8 Uvuvi).

## 3.0 KUTANGAZA FURSA NA KUTATUA CHANGAMOTO ZA UWEKEZAJI NA BIASHARA

### 3.1 Wadau Waliohudumiwa na Dawati

Zaidi ya wadau wa Mifugo na Uvuvi 213 wametembelewa/kukutana na kupewa ushauri wa kitaalam, vikiwemo viwanda vya kusindika maziwa, nyama, ngozi, samaki pamoja na wafugaji wa samaki katika vizimba na mabwawa.

Mikoa iliyotembelewa ni Dodoma, Njombe, Iringa, Mbeya, Tanga, Rukwa, Katavi, Songwe, Kigoma, Ruvuma, Manyara, Mwanza, Simiyu, Geita, Kagera, Mara, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Pwani, Lindi na Mtwara.

Wizara imeendelea kuongeza ushirikiano na Sekta Binafsi na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wadau wa maendeleo kama DALBERG, ANSAF, ASPIRE, WB, TADB, TPB Bank, NMB, CRDB, NIC, NSSF, PASS, TPSF na SAGCOT.

### 3.2 Mashirikiano katika Utendaji

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Dawati la Sekta Binafsi limesaini Hati ya Makubaliano na Taasisi ya Dalberg na ANSAF (*Agricultural Non-State Actors Forum*) na utekelezaji wa makubaliano hayo umeanza. Ushirikiano huu umeanza kwa kufanya tathmini ya mnyororo wa maziwa nchini ambao umeshirikisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bodi ya Maziwa, NBS, Dalberg na ANSAF. Taasisi hizi zitaongeza nguvu katika mpango kazi wa Dawati (Private Sector Desk Action Plan)

### 3.3 Makubaliano ya Viwanda vya Kimkakati vya Maziwa

Dawati kwa kushirikiana na Idara ya Sera na Mipango ya Mifugo iliandaa Mpango wa Utekelezaji (*Operational Plan*) wa viwanda vya maziwa. Aidha, Dawati limewezesha Wizara kuingia katika Makubaliano (MoU) na Viwanda Vinne vya kiutekelezaji vinavyosindika maziwa yanayokaa muda mrefu bila kuharibika (Ultra Heat Treatment – UHT) ambavyo ni ASAS LTD, Tanga Fresh Ltd, MilkCom Ltd na AZAM Dairy Products. Lengo ni kuongeza usindikaji wa Maziwa kutoka lita **154,100** hadi lita **284,500** kwa siku, sawa na ongezeko la lita **130,500** kwa viwanda vyote kufikia Disemba 2019. AZAM.

### 3.6 Viwanda vya Samaki vya Kanda ya Ziwa

Dawati lilishiriki katika mazungumzo ya kutafuta muafaka wa Kibali cha Mionzi kinachotolewa Tume ya Mionzi Tanzania (TAEC) kwa Samaki wanaosafirishwa kutoka katika viwanda vya samaki vya Kanda ya Ziwa kwenda nje ya nchi. Wasafirishaji walikuwa wanalazimika kupeleka sampuli za samaki Arusha kwa ajili ya kupima na kupatiwa kibali cha kusafirisha kila mzigo wa samaki nje ya nchi. Upimaji wa Mionzi nchini uko kisheria lakini haufanyiki katika nchi za Uganda na Kenya zinazovua samaki pia katika Ziwa Victoria na husafirisha katika soko moja na Tanzania. Aidha, upimaji huu haufanywi kwa samaki wanaoingizwa nchini. Dawati liliwasilisha lalamiko hili kwa Wizara na kikao kiliandaliwa kwa Taasisi husika. Kufuatana na kikao hiki TAEC wamefungua ofisi Kanda ya Ziwa kwa ajili ya kupima sampuli za samaki. Timu ndogo ya ufuatiliaji iliundwa kwa ajili ya kuandaa MoU na Wizara kukubaliana juu ya ukubwa wa sampuli, muda wa upimaji na gharama.

Aidha, Dawati liliwasilisha Wizarani changamoto ya *slot size* ya samaki iliyoruhusiwa kisheria ili kuhuisha udhibiti wa urefu wa samaki (slot size) 50-85 cm na nchi za Kenya na Uganda ambayo imetatuliwa.

### 3.8 Uvuvi katika EEZ

Dawati la Sekta Binafsi limekuwa likishiriki kutafuta wawekezaji wa Ukanda wa Kiuchumi wa Bahari (EEZ) katika Bahari. Kwa sasa, Dawati limefanya mazungumzo na wawekezaji wa Mbweni JKT wenye meli mbili zenye urefu wa mita **24** na **22** zilizotaifishwa na serikali baada ya kukamatwa zikisafirisha madawa ya kulevya katika Bahari ya Hindi. Meli kubwa ina uwezo wa kubeba tani **40** za samaki na ndogo tani **20**. Dawati limetembelea na kujionea meli hizo. Baada ya kikao cha majadiliano, Wizara ilipendekeza Wizara ya Ulinzi iombe fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya matengenezo ya Meli hizi na kuendeshea mradi kwa kuambatisha andiko la mradi.

Aidha, kumefanyika mazungumzo na Mwekezaji wa jijini Dar es Salaam ambaye ameonyesha nia ya kufanya uvuvi wa EEZ kwa kushirikiana na wawekezaji kutoka nje ya nchi. Kwa sasa anaandaa andiko ili kupata tathmini ya mradi.

### 3.9 Kiwanda cha nyama cha TANCHOICE

Kuendelea kutatua changamoto ya kiwanja alichofanya ujenzi wa kiwanda cha nyama huko Soga Mkoa wa Pwani kuanzia mwaka 2017

### 3.11 KUSHUGHULIKIA HOJA ZA WAWEKEZAJI

| Na. | Wadau | Hoja | Hatua iliyochukuliwa |
|---|---|---|---|
| 1 | Kiwanda cha Nyavu A to Z | TBS kuchelewesha kuwapatia kiwanda cha nyavu A-Z kibali cha kuendelea na uzalishaji baada ya kukaguliwa. | Dawati liliongozana na Meneja wa Kiwanda cha A-Z makao makuu ya TBS -kibali kilitolewa |
| 2 | Silverlands | Kutozwa kwa kodi na TRA kwa bidhaa ya DL Metionine toka nje ambayo ni kiambatishi katika vyakula vya mifugo. | Wizara ilipeleka barua ya maombi ya kusamehewa kodi kwa Kamishna wa TRA yenye Kumb. Na. PD 122/186/01/95 ya tarehe 17 Decemba, 2018 - msamaha wa kodi ulitolewa |
| | | Katika usafirishaji wa vifaranga kupeleka Dar es Salaam kampuni ilipata vikwazo mara mbili vya malipo ya vifaranga hivyo | Ufafanuzi ulitolewa na maafisa wa Wizara na kuwaruhusu kuendelea na safari. |
| 3 | AKM Gliter | Kufuatilia mkopo wa TADB | Mkopo huu unaendelea kufuatiliwa |
| | | Kuomba msamaha wa kodi TRA kwa vifaa vilivyoagizwa kutoka nje na Kampuni kwa ajili ya uzalishaji wa kuku. | Dawati lifuatilia TRA lakini ikaonekana vifaa vilivyoagizwa havipo kwenye orodha ya msamaha hivyo vililipiwa. |
| | | Kuomba wizara ishughulikie makampuni 14 yasiyosajiliwa yenye kusambaza kuku aina ya Kroiler. | Wizara inaendelea kufuatilia kampuni hizi kujishughulisha na biashara bila kukamilisha taratibu |
| 4 | Farmbase Vs TRA mara 3 | TRA kuwatoza malipo ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa viuatilifu vya dawa ya kuogesha mifugo PARANEX | Malipo yalifanyika - maombi ni kufuatilia mabadiliko ya kodi kwa viuatilifu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5 | Marenga Millers Vs TBS | Mfumo wa ukaguzi wa bidhaa katika nchi inapotoka- *Pre-Shipment Verification of Conformity* (PVoC) ulichelewasha mzigo kutoka Uholanzi kwa Zaidi ya miezi miwili | Wizara iliandikia barua TBS kwa ajili ya ombi la kufanyiwa '*Destination Inspection'.* Pia kampuni ilishauriwa kuomba daraja A la ukaguzi wa mizigo yao kwa haraka |
| 6 | MilkCom (Dar Fresh) | Maombi TANESCO ya kuongezewa nishati ya umeme kufikia megawati 8 kulingana na mahitaji ya kiwanda yamechukua muda mrefu na ukatikaji umeme umekuwa mara kwa mara hivyo kuathiri ubora wa maziwa na shughuli za kiwanda. | TANESCO waliongeza megawati 5 na ahadi ya kufikisha 8 ilitolewa |
| | | Barabara ya kwenda kiwandani ilikuwa mbovu sana na wakati wa mvua magari yalikuwa yanakwama. | Barabara ilirekebishwa kwa kiwango cha changarawe na hivyo inapitika wakati wote |
| 8 | TALIRI- Tanga | Mfumo kutowaruhusu kukopa fedha kutoka kwenye Taasisi za fedha | Wameombewa kibali kutoka kwa Msajili wa hazina |
| 9 | Kiwanda cha AZAM | Kufungwa kwa kiwanda baada ya ongezeko la tozo ya maziwa yanayotoka nje ya nchi kutoka Tshs **150**/-hadi Tshs. **2,000**/- kwa lita. | Kushirki katika timu ya ushauri iliyowasilisha mapendekezo na serikali iliridhia AZAM kutozwa Tshs. **2,000**/ kwa kilo ya maziwa ya unga ambayo inazalisha lita 8 za maziwa ya maji hivyo kufanya tozo ya Tshs. 250/= kwa lita.<br><br>Kiwanda kilifunguliwa na kinaendelea kushirikiana na Wizara katika kuongeza usindikaji wa maziwa kutumia maziwa ghafi kutoka kwa wafugaji wa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. |
| 10 | Aquasol Limited | Upatikanaji wa hati miliki ya ardhi kutoka kwa Kamishna wa Kanda ya Ziwa na kukataliwa kwa hati ya | Wizara ililiandika barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kimila katika kupata mkopo toka TADB | ya Makazi - ufafanuzi ulitolewa kuwa Hati ya Kimila ina hadhi sawa na Hati Miliki ya Ardhi. |
| 11 | Viwanda vya Samaki vya Kanda ya Ziwa vya: Nile Perch Ltd, Omega Fish Ltd, Tanzania Fish Processors, Natures Fish Ltd, Victoria Perch Ltd na Supreme Perch Ltd (Vick Fish) | Uhitaji, gharama na upatikanaji wa Hati ya Mionzi (Radiation Certificate) kutoka Tume ya Mionzi Tanzania (TAEC) kulingana na Sheria ya Mionzi ya mwaka 2003 wakati nchi za Uganda na Kenya hazihitaji hati hiyo pamoja na soko ni moja na samaki ni kutoka Ziwa moja. | Kikao kilifanyika kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Viwanda na Biashara, TAEC na wadau wengine kwa ajili ya kujadili swala hili- TAEC imefungua ofisi Mwanza badala ya awali ya Arusha iliyokuwa inafanya zoezi kuchukua muda mrefu. |
| | | Ukubwa (Slot size) kuanzia sentimita 50- 80 unaokubalika kisheria wa samaki wanaovuliwa na kupelekwa viwandani | Wizara imeondoa ukomo huo ili kuleta ushindani wa kibiashara. |
| 12 | Wadau wa Uvuvi | Leseni za uvuvi kukatwa kila wilaya<br><br>Kukataliwa kupewa mikopo kwa wadau wa uvuvi na taasisi za fedha (mabenki) na wadau kushindwa kuweka akiba Benki | Marekebisho madogo ya kanuni ya uvuvi yalifanyika na sasa wavuvi wanaruhusiwa kukata leseni moja katika eneo moja la mavuvi (water body)<br><br>Kuratibu zoezi la ufunguzi wa Mvuvi Account katika Benki ya TPB ili kusaidia wadau wa uvuvi kuweka akiba ya fedha na kupata mikopo. |
| 13 | (Mwekezaji wa vizimba Mwanza) | Kufuatilia uwekezaji wa vizimba vya samaki. | Alipatiwa mkopo kwa ajili ya uwekezaji |
| 14 | West Kilimanjaro Dairy Product (WKDP) | Kiwanda kinaomba eneo la hekta tano ili kiweze kuwekeza kiwanda cha maziwa | Ufuatiliaji wa ombi hili unaendelea |

## 4.0 KUITANGAZA SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

### 4.1 Ushiriki katika maonesho

Dawati la Sekta Binafsi limekuwa likishiriki katika kazi mbalimbali za Wizara na Sekta Binafsi. Dawati limeshiriki katika maonesho ya Saba Saba ya mwaka 2019 katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam na Nane Nane 2019 katika Viwanja vya Nyakabindi Mkoani Simiyu na Viwanja vya Zuguni Mkoani Dodoma. Katika maonyesho yote Dawati limekuwa likikutana na wawekezaji na kushiriki katika kutoa mada za maendeleo ikiwa ni pamoja na kugawa vipeperushi kwa wadau wanaotembelea maonesho na ofisi ya Dawati. Pia, kuna mabango, fulana na kofia zinazotambulisha Dawati.

Aidha, Dawati limekuwa likishiriki kutoa mada za uwekezaji na fursa za sekta ya mifugo na uvuvi katika vyombo vya habari kama redio, TV na mitandao ya kijamii. Dawati limejitangaza kupitia vipindi vinavyorushwa na kupitia vipindi vinavyoandaliwa na Kitengo cha Habari cha Wizara na Kipindi cha ASDP II kilichoandaliwa na Wizara ya Kilimo. Jumla ya vipindi sita (**6**) vimeandaliwa kwa mwaka 2018/19 katika vyombo vya habari.

Vile vile, Dawati limekuwa likitoka katika Makala mbalimbali za magazeti ya serikali na binafsi kama Habari Leo, Mwananchi na *Daily News*.

**Mafanikio ya Dawati la Sekta Binafsi**

i) Kuandaa na kusimamia mandalizi Mipango ya Biashara (Business Plans) kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi za za NARCO, TALIRI, TAFICO na TVLA kwa ajili ya kupata mikopo na kuongeza uwekezaji;

ii) Kuandaa kanzidata (database) ya Mifufo na Uvuvi kwa ajili ya kuweka muundo wa utambuzi wa wafugaji na wavuvi. Kwa sasa, vyama vya Ushirika vya Wavuvi vimeingizwa katika mfumo kwa majaribio ya awali;

iii) Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa kutoa jumla ya shilingi **50,000,000**/= kwa Vyama vya Ushirika vitano (**5**) vilivyo katika halmashuri hiyo ili kuongeza mtaji wa uwekezaji;

iv) Kushiriki kwenye mijadala ya kisera iliyotoa fursa za kujengwa na upanuzi wa vya maziwa (Galaxy Food and Beverages), ngozi (ACE Leather, Necai), nyama (SAAFI, Necai, Ngulu Hill, TANCHOICE) na uvuvi ();

v) kama Ngulu Hill, upanuzi wa Kiwanda cha ngozi cha ACE Leather, Morogoro.

vi) , Kiwanda cha Maziwa cha kiwanda cha mabondo

**Changamoto za Utekelezaji**

i) Dawati kutokuwa na rasilimali za kuweza kufika katika eneo kubwa la nchi;

ii) Mikopo kutotolewa kwa wakati. Kuchelewa kutolewa kwa mikopo kutokana na Bodi ya Maendeleo ya Kilimo kuisha muda wake;

iii) Wavuvi na wafugaji kutokufanya shughuli zao kibiashara hivyo kupelekea kutopatiwa mikopo kirahisi na kutokupata faida (kutokuweka kumbukumbu katika shughuli zao);

iv) Biashara nyingi kutokufanya vizuri kutokana na changamoto ya usimamizi na muundo wa utaalamu wa kusimamia biashara hizo (Composition of Board of Directors); na

v) Taasisi za Fedha kutokuwa na wataalam wa ushauri kwenye maeneo ya biashara ya mifugo na uvuvi japo kuna fursa kubwa, hivyo, kuziona ni biashara zenye *risk* kubwa ya uwekezaji.